KEY DATES

Kwa nini hizi Siku 16??

Siku 16 za Harakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia unatumia siku 16 kati ya Siku ya Kimataifa ya Kutokemeza Ukatili Dhidi ya Wanawake (Novemba 25) na Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu tarehe 10 Desemba) ili kuchochea utokomezwaji wa aina zote za ukatili dhidi ya wanwake na kuwa vitendo vya kusababisha ukatili dhidi ya wanawake ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Kampeni ya Siku 16 inaleta mfumo wa haki za binadamu kwenye shina kiini cha kazi na kuitumia ili kuhakikisha serikali na watendaji wasio wa serikali wote kwa pamoja wanawajibika kwa vitendo dhidi ya wanawake .

Umuhimu wa tarehe 25 Novemba na tarehe 10 Desemba

SIKU YA KIMATAIFA YA KUTOKOMEZA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE TAREHE 25 NOVEMBA

Novemba 25 ilitangazwa kuwa ni Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake katika mkutano wa kwanza wa harakati za ukombozi wa wanwake kimapinduzi kwa Amerika ya Kusini na Visiwa vya Caribbean uliofanyika Bogota, Colombia, mwezi Juaitarehe 18-21, mwaka 1981. Mikutano hiyo ya harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduziilikuwa ni mikutano ya wanaharaki wa ukombaozi wa wanwake kimapinduzi kutoka Amerika ya Kusini waliokutana kila baada ya miaka 2-3 katika nchi mbali mabali za Amerika ya Kusini ili kubadilishana uzoefu na kutathmini hali ya vuguvugu la ukombozi wa wanawake.. Katikia Mkutano huu wa Kwanza, wanawake kwa utaratibu walipinga vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia kuanzia mauaji nyumbani, ubakaji, unyanyasaji wa kijinsia hadi kwenye ukatili wa serikali ikiwemo mateso na unyanyasaji wa wafungwa wa kisiasa.. Tarehe 25 Novemba ilichaguliwa kuadhimisha mauaji ya kikatili ya Madada wa Mirabal (Patria, Minerva na Maria Teresa) tarehe 25 Novemba mwaka, 1960 na utawala wa Kidikteta waRafael Trujillo katika Jamhuri ya Dominican . Mwaka Umoja wa Mataifa ulitambua rasmi tarehe 25 kama Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake Madada wa Mirabal ni akina nani?

Patria, Minerva, Maria Teresa na Dedé walizaliwa Ojo de Agua karibu na mji wa Salcedo, katika jiji la Cibao kwenye Jamhuri ya Dominican c. "Las Mariposas" (" vipepeo"), kama walivokuwa wakiitwa , walikuwa ni wanaharakati wa kisiasa na mfano kubwa ulioonekana wa upingaji wa Udikteta wa Trujillo. Walifungwa mara kwa mara, pamoja na waume zao, kwa ajili ya harakati zao za kimapinduzi kuelekewa usawa ba demokrasiaTarehe 25 Novembamwaka 1960, watatu kati ya madada wa Mirabal , Minerva, Patria na Maria Teresa waliuwawa, pamoja na Rufino de la Cruz, dereva wao, na wanachama wa jeshi la siri la Trujillo. Wanwake hao watatu walikuwa wakiendeshwa na Rufino kwenda Puerto Plata kutembelea waume zao walikokuwa kifungoni. Miili ya madada hao watatu ilipatikana katika chini ya genge ikiwa imevunjwa vunjwa na kunyongwa Habari za mauaji yao ya kikatili yalishtua na kukasirisha taifa na kusaidia katika kuanzisha kwa vuguvugu lakupinga utawala wa Trujillo Trujilloaliuwawa tarehe 30 mei, mwaka 1961 na utawala wake ukaangukia punde tu.

Madada wa Mirabal wamekuwa mifano ya upinzani maarufu na harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi. Katika miaka baada ya kifo chao, wamekuwa wakikumbukwa katika mashairi, nyimbo na vitabu. .Maonyesho ya mai zao yamewekwa vizuruiMakumbusho ya Taifa ya Historia na Geografiakatika Jamhuri ya Dominica, stempu zimetengezwa ili kuwakumbuka na shirika binafsi lniachangisha pesa ili kukarabati Makumbusho ya familia katika mji wao.. Tarehe 8 Machi mwaka 1997,Siku ya Wanawake Kimataifa sanamu ilifunuliwa juu ya mnara wenye urefu wa futi137- (ambao Trujillo aiujenga kwa heshima yake) kwenye mji wa Santo Domingo, unaonyesha taswira za madada hao wanne. Mchoro katika mnara huo umepewa kichwa cha habari (Wimbo kulekea Uhuru).

Kwa maelezo zaidi angalia maelezo ya kufikirika juu ya Madada wa Mirabal ya Julia Alvarez'I kwenye kitabu chake cha hadithi cha mwaka 1994 , "Wakati wa Vipepeo)s;" Bernard Diederich's book "Trujillo: Kifo cha Dikteta" na Madada wa Mirabal," in Connexions, an International Women's Quarterly, No. 39, 1992.

SIKU YA KIMATAIFA YA HAKI ZA BINADAMU, DESEMBA 10

Tarehe 10, watu na serikali duniani wanasherehekea kupituishwa kwa Azimio la Haki za Binadamu mwaka 1948 Katika kilele hiki katika historia ya kisasa , mataifa ya dunia yaliungana ili kujaribu kufukia moja kwa moja, athira za maujai ya halaiki yaliofanywa na Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Azimio hilo lilikuwa mojawapo ya mafanikio makubwa ya Umoja wa Mataifa na lilitoa falsafa ya msingi kwa nyaraka mbali mbali za kisheria kufuata Aazimio 217A (III) la Mkutano Mkuu linatangaza (Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu kama kigezo muhimu cha mafanikio ya watu wote na mataifa yote, hadi kwenye kila chombo cha jamii, na kulifanya Azimio hili kuwemo katka mawazo liweze kudumu kwa kufundisha na kuelimisha na kuinua heshima ya haki na uhuru..."

Mashirika na watu binafsi wanatumia Siku ya Haki za Binadamu kama fursa ya kuadhimisha utiwaji sahihi wa nyaraka ya kihistoria na kuinua misingi yake. Siku ya Haki za Binadamu, kulingana na Kamishina Mkuu wa Haki za Binadamu aliyepita, Mary Robinson,ni " ni tukio la kuomyesha kuwa misingi ya Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu yalikuwa siyo nadharia ."

Ili kupata nakala ya Azimio la Kimataifa juu ya Haki za Biandamu, tafadhali tembelea tovuti ya Umoja wa Mtaifa:
http://www.ohchr.org/

Tarehe Muhimu za Harakati za Ukombozi wa Wanawake Kimapinduz

SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU 29

Kuwatetea Wanawake Kutetea Haki ni Kampeni ya Kimataifa iliyozinduliwa mwaka 2004 kwa ajili ya kutambua na kulinda watetezi wa haki za binadamu kwa wanawake ambao ni wanaharakati wanaotetea utambuliwaji wa haki zote za binadamu kwa watu woteKampeni inadai kwamba wanawake wanaopigania haki za binadamu na wanaharakati wote wanaotetea haki za wanawake wanakumbana na ukiukwaji maalum kama sababu ya utetezi wao au jinsia yao.. Novemba29 ni siku ya kuwatambua wanawake watetezi wa haki za binadamu, na ni siku ya kuadhimisha unaharakati, utetezi na vitendo vya kijasiri katika upingaji. Kampeni inalenga katika kulinda haki na athari za udhalilishaji wa serikali na watendaji wengine wasio wa serikali (m ikiwemo familia na jamii) ongezeko la utawala wa kijeshi na misimamo mikali, na njia nyingi ambazo watetezi wamekuwa wakilengwa kwa sababu ya mahusiano ya kingono, ikiwemo mtizamo wa kuwa msagaji au shoga.

Kwa maelezo zaidi, angalia tovuti ya kampeni ya wanawake watetezi wa haki za binadamu t http://www.defendingwomen-defendingrights.org/ *kwa picha za luninga,tahadhari za hatua, taarifa, na machapisho mengine unayoweza kutumia katika kusherehekea Siku ya Kimataifa ya Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu katika jamii yako.*

MAUAJI YA MONTREAL DESEMBA 6

Tarehe Desemba 6, mwaka 1989, mwanaume wa miaka 25 aliyejulikana kwa jina la Marc Lepine aliingia katika Chuo Kikuu cha Shule ya Ukandarasi wa Majengo Montreal na bunduki ndogo. Alianza kufyatua risasi mfululizo ambazo aliwauwa wanawake 14 na kuwajeruhi wengine 13: wanawake 9 na wanaume 4.. Lepine aliamini kuwa ni kwa sababu ya wanafunzi wanawake ndiyo maana alikataliwa kujiunga na shule ya ukandarasi. Kabla hajajiua , aliacha barua yenye maelezo yaliyoonyesha uhasama na wanaharakati wanawake kimapindizi na pia orodha ya wanawake 19 maarufu aliowadharau

Wanawake kumi na nne waliouwawa katika mauaji hayo walikuwa : Anne-Marie Edward, Anne-Marie Lemay, Annie St. Arneault, Annie Turcotte, Barbara Daigneault, Barbara Maria Klueznick, Genevieve Bergeron, Helen Colgan, Maud Haviernick, Maryse Laganiere, Maryse Leclair, Michele Richard, Natalie Croteau na Sonia Pelletier.

Wanawake hawa wakawa mfano, wawakilishi wa kutisha wa kutokutendewa haki kwa wanawake. Vikudi vya wanawake chini viliandaa maandamano, kumbukumbu na ibada za kuwakumbuka marehemu. Kulikuwa na ongezeko la misaada ya mipango ya elimu na rasilimali ili kupunguza ukatili dhidi ya wanawake. Serikali za shirikisho na za mikoa zilitoa ahadi za kukomesha ukatili dhidi ya wanawake. Mwaka 1991, Serikali ya Canada ilitenga tarehe Desemba kama Siku ya Kitaifa ya Kuwakumbuka na Kuchukua Hatua juu ya Ukatili Dhidi ya Wanawake.. Mwaka 1993, shirika linalojiita Muungano wa Des. 6 ulianzisha mfuko wa kusaidiana kwa wanawake wanaojitoa kwenye maeneo yenye ukatili ili kuanzisha maisha yao nay a watoto wao kwenye maeneo salama.. Pia mwaka1993 kampani iliyojulikana kama UVUMILIVU SIFURI ulizinduliwa na kutoa fursa kwa wanaume kuonyesha mshikamano na wanawake dhidi ya ukatili. Kama sababu ya moja kwa moja ya mauaji„ wanwake wengi wa wahanga walinzisha vikundi ili kupinga shria ya silaha na kuinua uelewa juu ya muendelezo wa ukatili dhidi ya wanawake..

Kwa taarifa zaidi, angalia "Mauaji ya Montreal " kilichoandikwa na Louise Malette & Marie Chalouh, Gynergy Books/Ragweed Pr; ISBN: 0921881142 au tembelea tovuti ya Wanaume kwa Mabadiliko kwenye http://www.chebucto.ns.ca/CommunitySupport/Men4Change/

Siku za Kimataifa zilizotengwa na Umoja wa Mataifa zinazoangukia ndani ya Siku 16

Kupitia maazimio yaliyokubaliwa na Mkutano Mkuu, Umoja wa Mataifa ulitenga siku za kutambua matukio au masuala muhimu.. Unaweza kupata orodha ya tarehe hizi kwa kupitia http://lib-unique.un.org/lib/unique.nsf/Link/R02091. Kwa taarifa , tumetoa hapo chini orodha ya tarehe zilizotengwa na Umoja wa Mataifa zinzoangukia kwenye Kampeni ya Siku 16.. Hatujaiweka tarehe 25 25 Novemba na tarehe 10 Desemba kama zilivoelezewa kwa kina hapo juu. Maelezo yote hapo chini yamechukuliwa moja kwa moja kutoka kwenye tovuti ya Umoja wa Mataifa na unweza kutembelea mitandao mingine ili kufahamu zaidi juu ya kila siku.. Kama kuna shughuli kwa ajili ya Kampeni ya Siku 16 unayodhani itaende sambamba na hizi siku, zingatia kuziunganisha kwenye utetezi wako ili kubainisha muingiliano huo.

ISIKU YA KIMATAIFA YA MSHIKAMANO NA WATU WA PALESTINA NOVEMBA 29

IMwaka 1977, Mkutano Mkuu ulitoa mwito wa uhifadhi wa tarehe 29 Novemba kama Siku ya Kimataifa ya Mshikamano na Watu wa Palestina (azimio 32/40 B). Siku hiyo mwaka 1947, Mkutano Mkuu ulipitisha azimio la kuitenga Palestine (azimio 181 (II)).

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea,tovuti ya Umoja wa Mataifa: http://www.un.org/depts/dhl/palestinian/index.html

SIKU YA UKIMWI DUNIANI DESEMBA 1

Siku ya Ukimwi Duniani nafanyika kila mwaka tarehe 1 Deemba . Siku hii inafikia kilele cha mwanzo wa kampeni ya kila mwaka inayotia moyo msaada wa kijamii kwa uundwaji wa mipango ya kuzuia ueneaji wa maambukizi ya Ukimwi. na kutoa elimu na kuinua uelewa wa masuala yanayozunguka VIRUSI VYA UKIMWI/UKIMWI.Kwanza mwaka 1988 mkutano ulitoa mwito kwa moyo wa kuvumilia na zaidi ubadilidhsanji wa taarifa juu ya VIRUSI VYA UKIMWI/UKIMWI Siku ya Ukimwi Duniani inatumika kama njia ya kuboresha juhudi za kimatafa kukabili changamoto za janga la UKIMWI

Kwa taarifa zaidi juu ya Siku ya Ukimwi Duniani, wasiliana na Kamati Tendaji ya

t UNAIDS , 20 avenue Appia, 1211 Geneva 27, Switzerland, ph: +41 (22)791 3666, nukushi(41-22)791 4187, baruapepel: unaids@unaids.org, tovuti: http://www.unaids.org

CWGL ilitoa taarifa , "Kuimarisha Upinzani:Kupambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na VIRUSI VYA UKIMWI NA UKIMWI," inayolenga kwenye maeneo ya ushirikiano katika jamii, haki za binadamu na migogoro ya afya ya jamii kwenye ukatili dhidi ya wanawake na VVU/UKIMWI. Kwa taarifa zaidi, tembelea
http://www.cwgl.rutgers.edu/globalcenter/publications/strengthening.htm

SIKU YA KIMATAIFA YA KUKOMESHA UTUMWA, DESEMBA 2

Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Utumwa, tarehe 2 Desemba, inakumbuka tarehe ya kupitishwa kwa Mkataba wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa e Ukandamiza kwenye Biashara ya Binadamu na Unyonyaji katika Biashara ya Ukahaba kwa Wengine(azimio 317 (IV) la tarehe 2 Desemba mwaka 1949). Kwa azimio 57/195 la Desemba 18 mwaka 2002, Mkutano ulitangaza mwaka 2004 kama Mwaka wa Kimataifa wa Kuadhimisha Harakati dhidi ya Utumwa na Ukomeshaji wake.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya Umoja wa Mataifa http://www.un.org/depts/dhl/slavery/

SIKU YA KIMATAIFA YA WATU WENYE ULEMAVU DUNIANIDESEMBA

Kila mwaka utunzaji wa Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu, tarehe 3 Desemba, unalenga kuinua ufahamu wa masuala ya ulemavu na kuhamasisha msaada wa utu, haki na ustawi wa watu wenye ulemavu..Pia inalenga katika kuongeza uelewa wa faida zinazoweza kupatikana kwa kuwashirikisha watu wenye ulemavu katika nyanja zote kisiasa, kiuchumi, kijamii na maisha ya kiutamduni.. Mada ya siku inajikita kwenye lengo la ushiriki kamilifu na usawa katika kufurahia haki za binadamu na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu kwenye jamii, iliyoanzishwa na Mpango Wa Hatua juu ya Watu Wenye Ulemavu Duniani, na kuchukuliwa na Mkutano Mkuu mwaka 1982.

Kwa taarifa zaidi juu ya Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu,tafadhali tembelea tovuti ya Umoja wa Mataifa: http://www.un.org/disabilities/

SIKU YA KUJITOLEA KIMATAIFA KWA MAENDELEO YA KIJAMII NA KIUCHUMI, DESEMBA 5

Siku ya Kujitolea Kimataifa (IVD)inatoa fursa kwa wanaojitolea- ikiwemo mashirika na watu binafsi kufanyakazi pamoja kwenye miradi na kampeni zinazokuza mchango wao kwenye maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwenye ngazi ya jamii, taifa na kimataifa.. Kwa kuunganisha msaada wa Umoja wa Mataifa na nguvu ya jamii, , IVD ni fursa pekee kwa mawakala wa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, vikundi vya kijamii, na mashirika binafsi na wanaojitolea –ikiwemo mshirika kufanyakazi pamoja ili kufikia malengo maalum. IVD ilianzishwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa mataifa kupitia Azimio namba n 40/212 tarehe 17 Desemba mwaka 1985. Tokea wakati huo, serikali, Umoja wa Mataifa na mashirika ya kijamii yameweza kuungana na wanaojitolea duniani ili kusherehekea Siku hii tarehe 5 5 Desemba.

Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti ya Umoja wa Mataifa kwa Wanaojitolea: http://www.unv.org/ au http://www.un.org/en/events/volunteerday/

SIKU YA KIMATAIFA YA USAFIRI WA ANGA DESEMBA 7

Lengo la sherehe za kidunia ni kutoa na kuimarisha uelewa wa dunia juu ya umuhimu wa siku ya kimataifa ya usafiri wa anga katika maendeleo ya Serikali kijamii na kiuchumi, na jukumu la ICAO katika kukuza usalama, ufanisi na utaratibu wa usafiri wa anga kimataifa.

Kwa taarifa zaidi temebelea : http://www.icao.int/icao/en/aviation_day.htm

SIKU YA KUPAMBANA NA RUSHWA DUNIANI, DESEMBA 9

Kwa azimio namba 58/4 la tarehe 31 Oktoba mwaka 2003, Mkutano Mkuu uliteua tarehe 9 Desemba kama Siku ya Kupambana na Rushw a Duniani Uamuzi huu ulichukuliwa ili kuongeza uelewa wa jamii juu ya rushwa na jukumu la Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya kuzuia na kupambana na Rushwa.

Kwa taarifa zaidi , tembelea tovuti ya Umoja wa Mataifa: http://www.un.org/depts/dhl/events/anti_corruption/

Translated by Festa Andrew Mwanyingili, Women's Dignity